

Viacheni vyote vikue hata wakati wa mavuno;" maana yake nini?

SWALI: Nini maana ya huu mstari? "Mathayo 13:30 Viacheni vyote vikue hata wakati wa mavuno; na wakati wa mavuno nitawaambia wavunao, Yakusanyeni kwanza magugu, myafunge matita matita mkayachome; bali ngano ikusanyeni ghalani mwangu. "

JIBU: Mfano huu Bwana alioutoa unahu siku za mwisho, na kumbuka siku za mwisho ndio hizi tunazoishi sasa mimi na wewe, kwamba Bwana atatumua wavunaji watakaovuna watu, sasa ili kuelewa hawa wavunaji ni wakina nani hebu tusome mstari ufuatao..

Mathayo 9:37 " Ndipo alipowaambia wanafunzi wake, Mavuno ni mengi, lakini watenda kazi ni wachache.

38 Basi mwombeni Bwana wa mavuno, apeleke watenda kazi katika mavuno yake."

Unaona hapo, siku hizi za mwisho, wahubiri ndio wavunaji, na siku hizi za mwisho Bwana amesema atawatuma wengi, wa ukweli na wauongo, ambao watawavuna watu wote walioko ulimwenguni (waovu na wema), wale walio waovu (wanaofananishwa na magugu) watafungwa matita matita (yaani watafungwa katika madhehebu mbali mbali) na

Viacheni vyote vikue hata wakati wa mavuno;" maana yake nini?

watasubiria kutupwa katika lile ziwa liwakalo moto na kiberiti,
kwasababu ni magugu.

Kama unapenda uasherati, utapata muhubiri atakayekufariji katika
uasherati wako, vivyo hivyo na mambo mengine maovu, utapata
wahubiri na waalimu na makanisa yanayochukuliana na hayo mambo.

Lakini wale walio wema(*yaani zile ngano njema*) zitakusanywa pamoja
na kuhifadhiwa ghalani (*na ghalani ni mbinguni*), wale walio tayari
kufumbua macho yao waone, kufumbua masikio yao wasikie, Bwana
anawakusanya katika siku hizi za mwisho kupitia wahubiri wake
waaminifu na wa kweli na kuwaweka tayari kwa ajili ya unyakuo.

Je! Na wewe umejiandaaje? Huu ni wakati wa
kukusanywa, Unakusanywa wapi leo? Kwenye dhehebu lako? au katika
Neno la Mungu?.

Kanisa/muhubiri asiyekuhubiria kwamba Ibada za
sanamu,ulevi,ulavi,ulawiti,uongo,rushwa,wizi,masturbation,
chuki,usengenyaji,uvaaji vibaya, ni tiketi ya kwenda motoni, basi huyo ni
mvunaji ametumwa kukufunga katika tita lake, na kukupeleka motoni,
Biblia inasema mtu asipozaliwa mara ya pili kwa maji na kwa Roho
hawezi kuuona ufalme wa mbinguni na pasipo huo UTAKATIFU hakuna

Viacheni vyote vikue hata wakati wa mavuno;" maana yake nini?

mtu atakayemwona Mungu.

Ubarikiwe!

Ikiwa utahitaji msaada zaidi ya mafundisho ya kila
siku/maombezi/ubatizo/ushauri basi wasiliana nasi kwa namba zetu hizi
+255693036618/+2557890001312

Au jiunge na makundi yetu ya mafundisho ya kila siku kwa kwa njia
ya **Whatsapp kwa kubofya hapa >>> WHATSAPP GROUP**

Mada zinazoendana:

HUIJUI KAZI YA MUNGU, AFANYAYE MAMBO YOTE.

INJILI KULINGANA NA TEKNOLOJIA.

LULU YA THAMANI.

MSHIKE SANA ELIMU.

Viacheni vyote vikue hata wakati wa mavuno;” maana yake nini?

MAISHA YETU NI MILKI YA YESU KRISTO.

TUZIJARIBU HIZI ROHO.

Rudi Nyumbani:

Share on:

WhatsApp

[Print this post](#)